

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA SEPTEMBER 2017 NA MWELEKEO WA OKTOBA, 2017

Dondoo za Oktoba, 2017

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria vya hali ya hewa na mwenendo wa mvua katika mwezi uliopita na mwelekeo wa viashiria na hali ya mvua kwa mwezi Oktoba 2017 nchini.

- a) Mvua za Msimu katika ukanda wa Pwani ya kaskazini zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza ya mwezi Oktoba, 2017
- b) Japokuwa mvua za msimu zimeshaanza katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, vipindi kadhaa vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo katika kipindi hiki.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA SEPTEMBER, 2017

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2017 baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria yamepata mvua za msimu wakati yale maeneo ya ukanda wa Pwani ya kaskazini na maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini mashariki yalipata mvua zilizo nje ya Msimu.

2.0 MATAZAMIO OKTOBA, 2017

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la bahari la chini ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya kati ya Kitropiki ya bahari ya Pasifiki na joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevuunyevu kutoka mashariki kuelekea katika maeneo ya Pwani ya nchi na hivyo kuleta mvua katika maeneo hayo. Hali ya joto la bahari la chini ya wastani eneo la pwani ya Angola, inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevuunyevu kutoka magharibi kuelekea katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na kuleta mvua na ngurumo.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA MWEZI OKTOBA, 2017

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2017.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Mvua na ngurumo zinatarajiwa hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2017.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususani maeneo ya mkoa wa Kigoma katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2017.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa na Mbeya): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu.

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**